# WANAWAKE na ARDHI

Ardhi ni Uhai

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

TOLEO LA 3

MACHI 2020


# BAADA YA DHIKI NI FARAJA:
## USHINDI WA MJANE ALIYEDHULUMIWA HAKI YAKE

*Na Alpha Visible Community Development (AVCD)*



Baadhi ya jamii nchini Tanzania zina mila na desturi ambazo ni kandamizi dhidi ya wanawake, wajane, yatima na walemavu. Mila na desturi zinakuwa kandamizi zaidi katika umiliki wa mali na rasilimali, ardhi ikiwa ni mojawapo. Tumeshuhudia Watoto wa kike wakikosa haki ya kurithi mali za wazazi wao kwa sababu tu "wataolewa" na watakwenda kupata na kumiliki mali wakiwa kwa waume zao. Ingawa uhalisia ni kuwa hata huko kwa waume zao hawapati haki hii ya kumiliki.

Katika maeneo mengi nchini kilichobainika ni kuwa mwanamke ana haki ya kulima na kuvuna na ukweli ni kuwa vijijini wanawake ndio wazalishaji wakubwa wa chakula na mazao mengine ukilinganisha na wanaume. Inapofika kunufaika na mazao waliyoyatolea jasho wanaume wamekuwa ndio wafanya maamuzi wenye nguvu zaidi. Mifano ya wajane waliofukuzwa na

*Inaendelea uk. 4*

YALIYOMO


- BAADA YA DHIKI NI FARAJA: USHINDI WA MJANE ALIYEDHULUMIWA HAKI YAKE — 1 & 4
- VIONGOZI WA VIJIJI NGUZO MUHIMU UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE — 3-4
- MAFUNZO YA HAKI ZA ARDHI YAREJESHA ARDHI NA WATOTO — 5
- MACHAPISHO YAWA CHACHU YA UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE — 6
- MSAADA WA KISHERIA WATOA AHUENI KWA WANAFAMILIA — 7
- VICOBA YATUMIKA KUTETEA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE — 8
- WANAWAKE WA KIMAASAI WANUFAIKA NA ARDHI — 10-11
- MILA KANDAMIZI KIKWAZO KWA WANAWAKE KUMILIKI ARDHI — 12-13
- NAFASI YA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI — 14-15



*Cathbert Tomitho*
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Utafiti na
Utetezi wa Haki za Ardhi

# WANAWAKE na ARDHI

Hili ni toleo la tatu katika mtiririko wa jarida hili la "Wanawake na Ardhi", katika toleo hili masuala kadhaa yamejadiliwa ambayo ni pamoja na mafanikio yanayoridhisha katika utetezi wa haki haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo hususani wanawake. Mafanikio haya yanatokana na mafunzo kuhusu haki za ardhi yanayotolewa na taasisi kumi na mbili zinazotekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika wilaya za Kiteto, Iringa, Morogoro, Kilolo, Arusha, Meru, Singida, Mufindi, Kilosa na Babati. Mradi huu unafadhiliwa na shirika la Foundation for Civil Society.

Mojawapo ya makala iliyojadiliwa katika jarida hili ni namna Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinavyoweza kulinda haki za ardhi kwa wanawake pale zinapotekelezwa ipasavyo kwenye maeneo ya vijijini na mijini. Kuna mifano kadhaa inayoonesha jinsi ambavyo Sheria hizi zimetumika kuwapatia haki wanawake waliodhulumiwa ardhi zao zaidi ya miaka tisa iliyopita. Vilevile kuna makala zilizojadili kuhusu msaada wa kisheria na unavyoweza kuimarisha na kuharakisha upatikanaji wa haki za ardhi kwa wanawake. Wanawake wengi wa vijijini wamekuwa wanufaika wakubwa wa msaada wa kisheria kutokana na hofu ya kusimama kidete kutetea haki zao na watoto wao kutokana na mila kandamizi ambazo zinawabana wanawake kutokurithi ardhi kutoka kwa wazazi wao na kutokuweza kumilikishwa ardhi pale inapotokea mume wake amefariki.

Vilevile kuna makala kuhusiana na matumizi sahihi ya vyombo vya utatuzi wa migogoro ya ardhi kama vile Baraza la Ardhi la Kijiji na Baraza la Kata katika kulinda haki za ardhi kwa wanawake. Makala hizi zinaonesha jinsi ambavyo wajumbe wa mabaraza walipopata mafunzo ya haki za ardhi waliweza kusimamia haki pasipo kuruhusu mfumo dume kutawala maamuzi yao. Kama tulivyosoma kwenye majarida yaliyopita viongozi wa kimila hususani makabila yale yenye mila kandamizi wameendelea kuwa chachu ya wanawake kupata haki za ardhi.

Rai yangu ni kuwa tunapoelekea kwenye maadhimisho ya siku ya wanawake duniani tarehe 8 Machi 2020 yenye kauli mbiu ya "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya sasa na Baadae". Tutumie kauli mbiu hii kuelewa kuwa tunapozungumzia usawa baina ya mwanamke na mwanaume hatuzungumzii kutengeneza tabaka la wanawake wanyanyasaji wa wanaume wala hatuzungumzii wanawake kulipa kisasi kwa wanaume kutokana na manyanyaso au ukandamizaji ambao wameupitia bali tunazungumzia umoja na ushirikiano katika kufanya maamuzi na kushirikiana katika masuala ya kijamii na kiuchumi kwa lengo la kuwa na familia na jamii bora itakayorithishwa na vizazi vijavyo.

Niwatakie wasomaji wote, Heri ya Mwaka Mpya 2020.
ARDHI NI UHAI



# VIONGOZI WA VIJIJI NGUZO MUHIMU UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE

*Na Iringa Civil Society Organizations (ICISO)*



*Pichani: aliyesimama ni Mwenyekiti wa kijiji cha Nyanzwa ndugu Samson Masambuli wakati akifungua mojawapo ya mafunzo yaliyofanyika kijijini.*

Taasisi ya Iringa Civil Society Organizations (ICISO – UMBRELLA) inatekeleza mradi kutoa elimu ya haki za ardhi kwa wanawake katika wilaya za Iringa na Kilolo za mkoani Iringa. Mradi huu unafadhiliwa na shirika la Foundation for Civil Society. Utoaji wa elimu hii unatokana na kukithiri kwa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa wanawake hususani kwenye kumiliki ardhi na mali nyinginezo. Katika wilaya hizi mbili kuna matukio mengi ya wanawake kunyanyaswa kutokana na kutokufahamu haki za wajibu wao katika kutetea haki zao za ardhi.

Mwezi Agosti 2019 ICISO ilifanya mafunzo ya uelewa wa Sheria za Ardhi hasa hasa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 pamoja na elimu ya uelewa kuhusiana na masuala ya ndoa na mirathi. Maeneo haya yalipewa kipaumbele kutokana na tafiti zilizofanywa na kubaini kuwa haya ndio maeneo makuu yanayowasumbua wanawake.

Mnamo mwezi Desemba 2019, Ndugu Sospeter Salia alifika katika Ofisi ya Serikali ya Kijiji cha Nyanzwa, wilaya ya Kilolo kwa ajili ya kumshitaki Ndugu Wille Nyambasa aliyekuwa anamdai Tsh. 270,000/=. Ndugu Nyambasa hakuwa na fedha hizo, hivyo alienda ofisi ya serikali ya Kijiji kwa ajili ya kuweka rehani nyumba yake ili aweze kupewa mkopo. Kulingana na tathmini ya viongozi nyumba hiyo ilikuwa na thamani ya Tsh. 850,000/=.

*Inaendelea uk. 4*

›› Inatoka uk. 1

shemeji zao kutoka kwenye nyumba na mashamba waliyoyatolea jasho kuyapata yeye na mumewe kabla hajafariki.

Pamoja na uwepo wa Sera na Sheria zenye vipengele vinavyompa haki mwanamke ya kupata, kutumia, kuuza, kugawa na kumiliki ardhi lakini bado unyanyasajі na ukiukwaji wa haki za wanawake unaendelea kwenye mikoa, wilaya na vijiji mbalimbali nchini. Kwa mfano kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kinakataza matumizi ya mila na desturi zinazowanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu njia halali za kumiliki, kukalia au kutumia ardhi ni batili hivyo hazipaswi kutumika katika usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Taasisi isiyo ya kiserikali ya Alpha Visible Community Development (AVCD) inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa kupitia ufadhili wa shirika la Foundation for Civil Society. Mradi huu unahusisha kutoa elimu ya haki za ardhi kwa wanawake kupitia njia za sanaa. Elimu inayotolewa na taasisi hii imeweza kuwasaidia wasichana na wanawake ambao hapo kabla hawakufahamu wafanye nini ili kupata haki zao ambazo zilishapotea kutokana na kutokufahamu wajibu wao kwa mujibu wa sheria za taratibu nyingine.

Mojawapo ya mfano wa wanawake ambao wamenufaika na elimu hii ni Bi. Dorice P. Mbaluka mwenye umri wa miaka 27 mkazi wa Kijiji cha Luhindo, wilayani Kilolo. Bi. Dorice ni mjane aliyefiwa na mumewe Novemba 2, 2015. Bi. Dorice anaeleza kuwa;

*"...Siku saba tu baada ya mazishi ya marehemu mume wangu. Shemeji zangu walikuja kuchukua vyombo vya ndani vikiwemo; kitanda na magodoro vitu ambavyo tulivinunua pamoja na mume wangu. Vilevile waliuza na shamba la ekari mbili lililokua tegemeo letu katika kilimo. Baadae tena walikuja na kuuza nyumba na kunilazimisha kutia saini ya kukubali kuuza nyumba. Nilikataa shuruti yao ndipo waliponikataza kufanya maendelezo kwenye ardhi yangu na katika nyumba yangu..."*

Manyanyaso na ukiukwaji huu wa haki za Bi. Dorice uliibuliwa wakati wa mafunzo kupitia mkutano wa hadhara uliofanyika Septemba 2019. Taasisi ya AVCD ilitoa elimu ya haki za ardhi pamoja na kumpa Bi. Dorice ushauri wa kisheria ikiwa ni pamoja na kukutana na Baraza la Ardhi la Kijiji ili apewe haki ya kurudishiwa ardhi yake pamoja na kumiliki nyumba aliyojenga na marehemu mumewe.

Dorice alifungua shauri katika Baraza la Ardhi la Kijiji ambapo mgogoro huo ulisuluhishwa kwa kumuhusisha Baba Mkwe wake na ndugu wengine wa mume wake. Mpaka kufikia Januari 2020 Baraza la Ardhi la Kijiji lilihitimisha shauri husika kwa kuamua kuwa Bi. Dorice arudishiwe mali zilizochukuliwa pamoja na kuendelea kuishi kwenye nyumba ambayo hapo awali ndugu za mumewe walitaka kuiuza kwa lazima. Kwa sasa, Bi. Dorice na familia yake wanaishi kwa amani na furaha baada ya kuweza kuipata haki yao ambayo ilikuwa inadhulumiwa na watu wachache kwa kutumia mila na desturi kandamizi.

›› Inatoka uk. 3

Mwenyekiti wa kijiji cha Nyanzwa Ndugu Samson Masambuli kabla ya kuridhia nyumba hiyo kuwekwa rehani alitaka kufahamu kama mke wa Ndugu Nyambasa alikuwa na taarifa kuhusiana na nyumba hiyo kuwekwa rehani na kama alikuwa ameridhia na ataweka saini kwenye nyaraka za uwekaji rehani. Uamuzi wa Mwenyekiti kutaka kufahamu kama mke wa muweka nyumba rehani anafahamu ulitokana na mafunzo aliyoyapata kutoka taasisi ya ICISO ambayo ilitoa mafunzo kuwa kifungu cha 114 cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kinatoa ulinzi kwa mali ya ndoa pale inapowekwa rehani kwa kuainisha kwamba rehani itakuwa halali endapo itakuwa na saini inayoonyesha mke au wake kuridhia uwekaji wa rehani wa nyumba au ardhi hiyo.

Vilevile kifungu cha 8 cha Sheria ya Rehani namba 17 ya mwaka 2008, kinazungumzia wajibu wa mkopaji kumjulisha mkopeshaji kuwa ana mke na ameoa, hivyo ni muhimu kwa mkopaji kutoa taarifa kuwa yeye ana mke au mume.

Kutokana na elimu hii imekuwa rahisi hata kuepuka utapeli wa watu kudhulumiwa nyumba, ardhi na mali nyingine kutokana na kuepuka kufanya mauzo, uwekaji rehani na hata kutokufanya malipo pasipo kuwashirikisha viongozi wa vijiji pamoja na wanawake na watoto. Halikadhalika elimu ya utambuzi wa Sheria za Ardhi na haki za wanawake umesaidia katika kupunguza na kuondoa kabisa ujanja na utapeli uliokuwa unafanywa na baadhi ya viongozi wa vijiji ambao sio waadilifu ambao walikuwa wakiwadhulumu wanavijiji haki zao kutokana na kutokufahamu haki zao kwa mujibu wa sheria.

# MAFUNZO YA HAKI ZA ARDHI YAREJESHA ARDHI NA WATOTO

Na Inter Religious VICOBA



Pichani: Bi. Halima Yasin Ramadhani akilima katika shamba lake la mahindi

Mtandao wa IR VICOBA Singida unatekeleza mradi wa kuwawezesha wanawake kufahamu haki zao ikiwemo haki ya kupata kutumia na kumiliki ardhi katika Manispaa ya Singida kupitia ufadhili wa shirika la Foundation for Civil Society. Moja ya sababu ya msingi ya kutekeleza mradi huu ni kutokana na wasichana na wanawake waishio mijini na pembezoni mwa miji kutokuwa na taarifa sahihi kuhusu haki zao za kumiliki ardhi na mali nyingine. Ukosefu huu wa taarifa sahihi unatokana na elimu duni ambayo wanawake walio wengine wanayo katika maeneo mengi ya mkoa wa Singida. Hali hii inathibitisha ule msemo wa *"kutafuta haki usiyoijua ni jambo lisilowezekana"*.

Changamoto hii ya kielimu na utambuzi wa haki imewafanya wanawake wengi kubaki nyuma kimaendeleo japokuwa ndio wazalishaji wakubwa katika shughuli za kilimo, ufugai na shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinazoingiza kipato kwenye familia zao. Hii ni tofauti na wanaume ambao baadhi yao wamekuwa wakizikimbia familia zao kwa sababu ya kwenda kutafuta fedha nje ya maeneo ya majumbani kwao.

Katika utekelezaji wa mradi huu taasisi ya IR Vicoba imekuwa ikiwasaidia wanawake walio wengi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakipitia manyanyaso ya kutokufahamu haki zao za ardhi. Mfano mmojawapo ni wa Bi. Halima Yasin Ramadhani mwenye umri wa miaka 39 mkazi wa kata ya Mungumaji. Bi. Halima ni mjane mwenye watoto sita. Baada ya kufiwa na mume wake alianza kupokea vitisho kutoka kwa ndugu za marehemu mume wake wakishinikiza aondoke katika nyumba aliyokuwa akiishi na mume wake huku wakimtaka awaache watoto wao. Vitisho na mashinikizo ya wakwe zake yalimfanya Bi. Halima kuishi kwa hofu na kushindwa kujihusisha na uzalishaji mali ikiwemo kilimo kutokana na katazo la kutokutumia mashamba ya familia. Bi. Halima aliishi kwenye manyanyaso haya kwa takribani miaka minne.

Mnamo tarehe 05/08/2019,Bi. Halima alipata mafunzo ya Sheria za Ardhi na taratibu za utatuzi wa migogoro ya ardhi. Baada ya mafunzo aliweza kupeleka shauri lake katika Baraza la Kata na kufanikiwa kushinda hivyo kurejeshewa mashamba yake. Mpaka sasa,Bi. Halima yupo huru na watoto wake na amefanikiwa kulima mahindi katika ekari tatu na nusu za hilo eneo.

Bi. Halima anashukuru sana kwa kuipata hii elimu kwasababu imewawezesha hata wanawake wenzake katika Kata ya Mungumaji kuwa jasiri katika kutetea haki zao pale wanaponyanyaswa. Bi.Halima anasema;

*"...Naomba elimu zaidi iendelee kutolewa kwani ndio iliyofanya hata wakwe zangu waridhie niendelee kutumia ardhi niliyoachiwa na mume wangu ..."*

# MACHAPISHO YAWA CHACHU YA UTETEZI WA HAKI ZA WANAWAKE

*Na Knowledge Attitude and Practice Foundation (KAPS)*

Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa ni wilaya inayokabiliwa na matukio mengi ya ukiukwaji wa haki za wanawake hususani kwenye umiliki wa ardhi na mali. Hii ni kutokana na mila kandamizi za makabila yanayoishi kwenye wilaya hii. Taasisi ya KAPs Foundation inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wazalishaji wadogo katika wilaya ya Mufindi, Iringa. Mradi huu unafadhiliwa na Foundation for Civil Society.

Makala hii itasimulia mojawapo ya mafanikio ambayo ni matokeo ya utekelezwaji wa mradi huu. Simulizi hii inamuhusu Bi. Diana Msimbwa mwenye umri wa miaka 50 wa Kijiji cha Tambalang'ombe, Kata ya Saadani, Wilaya ya Mufindi. Miaka nane iliyopita Bi. Diana alidhulumiwa ardhi ekari 3 na wajomba zake baada ya Mama yake mzazi kufariki.

Bi. Diana aliporwa ardhi hii kutokana na mila na desturi za jamii ya Wahehe ambazo haziruhusu mwanamke kurithi ardhi kutoka kwa wazazi pindi wanapofariki ardhi yote hurudi kwa wanaume walioko kwenye familia husika. Bi. Diana anaeleza zaidi;

> *"...Wajomba walivyonipora ardhi ya marehemu Mama yangu sikuwa na jambo la kufanya kwa sababu nilifahamu ndio mila za kabila letu la Wahehe ambazo hazimpi mwanamke nafasi ya kurithi ardhi...".*

Bi. Diana alifanikiwa kuhudhuria mafunzo ya haki za ardhi kwa wanawake yaliyokuwa yameandaliwa na taasisi ya KAPs Foundation. Katika mafunzo hayo alifanikiwa kupata kipeperushi kilichokuwa kinachambua haki za ardhi kwa wanawake kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi namba 4 na namba 5 za mwaka 1999. Niliposoma kile kipeperushi nilibaini kuwa Sheria za Ardhi zinampa mwanamke haki ya kupata, kutumia, kumiliki, kuuza, kununua, kugawa sawa sawa na haki aliyonayo mwanaume. Hapo ndipo alipoamua kumfuata mjomba wake na kumpatia kile kipeperushi akisome naye aelewe Sheria inasema nini kuhusu haki ya mwanamke.

> *"Niliamua kumpelekea kile kipeperushi mjomba wangu ili naye akisome kwa sababu niliamini kuwa ningemueleza kwa mdomo tu hasingenielewa na wala hasingefanya kile nilitaka akielewe ambacho nikunirudishia ardhi ya mama yangu..." anasimulia Bi. Diana*

Baada ya mjomba wake kusoma kile kipeperushi alielewa kilichokuwa kimeandikwa, hakuwa mbishi sana kwa sababu kipeperushi kilieleza mambo yote kwa uwazi. Mnamo tarehe 13.09.2019 Mjomba aliitisha kikao cha ukoo na kuwafafanulia ndugu zake kuhusu kilichoandikwa kwenye kipeperushi hivyo aliamua kumrudishia Bi. Diana shamba la ekari 3 ambalo lilichukuliwa kutoka kwake.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara Afisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Saadani, Bi. Gesela Shinyambala alieleza namna mafunzo ya haki za ardhi yalivyomsaidia Bi. Diana kupata haki yake ambayo alikuwa amedhulumiwa kwa miaka mingi. Afisa Mtendaji wa Kata aliwahimiza wanavijiji wote kuhudhuria mafunzo hayo pamoja na kujisomea machapisho ya masuala ya ardhi ili yawasaidie katika kumiliki ardhi zao kihalali na kuacha kudhulumu haki za watu wengine.



# MSAADA WA KISHERIA WATOA AHUENI KWA WANAFAMILIA



*Na Morogoro Paralegal Centre (MPLC)*

Ni wazi kwamba, hata kabla ya ujio wa Sheria za ardhi na 4 na 5 za mwaka 1999 zilikuwepo namna mbalimbali za watu kujipatia ardhi. Sheria za ardhi zimetambua namna za upatikanaji wa ardhi ambazo ni; kurithi, kununua, kupewa zawadi na kugawiwa na serikali. Pamoja na uwepo wa sheria zinazotambua aina hizi za kujipatia ardhi, bado kuna migogoro mingi sana inayotokea inayohusiana na ukosefu wa uelewa wa taratibu.

Shida Raphael (47) mkazi wa kitongoji cha Mkesa, kijiji cha Bonye, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, amekuwa na mgogoro wa ardhi na serikali ya kijiji juu ya umiliki wa shamba la urithi toka kwa marehemu baba yao Mzee Raphael Ngubi.

Mwanzoni mwa mwaka 2005, halmashauri ya kijiji cha Bonye kitongoji cha Sogea Mbele ilitangaza kugawa mashamba kwa wananchi. Kupitia mchakato huo Mzee Raphael alifanikiwa kupata ardhi yenye ukubwa wa ekari 49 kwa niaba ya watoto wake wawili Shida Raphael na Paulo Raphael kupitia mchakato rasmi wa ugawaji kwa ardhi uliosimamiwa serikali ya kijiji.

Mwaka 2006 Mzee Raphael alifariki, baada ya hapo watoto wa marehemu waliendelea kufanya shughuli za kilimo cha mpunga katika eneo hilo bila usumbufu. Tatizo lilianza mwaka 2010 ambapo wanae wawili Shida Raphael na Paulo Raphael walifika katika ofisi ya Kijiji cha Bonye kwa lengo la kuomba kukabidhiwa eneo hilo waliloachiwa na baba yao, jambo ambalo halmashauri ya kijiji hawakuafiki.

Licha ya Shida na Paulo kueleza namna baba yao alivyopata shamba hilo na kuonesha baadhi ya nyaraka zinazoonesha umiliki wa shamba hilo bado viongozi hao walitilia mashaka na kushindwa kuwapa msaada.

Hadi kufikia mwaka 2011, bado familia hiyo ilikua inahangaika kupata suluhu na Kijiji ambapo viongozi wa serikali ya kijiji walipeleka suala hilo katika mkutano mkuu wa kijiji ambapo wananchi wanaofahamu ukweli wa jambo hilo walisema shamba hilo ni mali ya Mzee Raphael hivyo watoto wake wakabidhiwe.

Mwaka 2016, Kituo cha Wasaidizi wa Kisheria Morogoro (MPLC) kilianza kutekeleza mradi wa ulinzi wa haki za ardhi kwa Wanawake na Wajasiriamali wadogo katika kijiji cha Bonye. Mradi huu ulihusisha kutoa mafunzo ya haki za ardhi kwa wanavijiji hususani wanawake ambapo Bi. Shida alifanikiwa kushiriki mojawapo ya mafunzo hayo ambapo alipata fursa ya kueleza kuhusiana na mgogoro wake wa ardhi uliokuwa unamkabili. Wanasheria wa MPLC walimkutanisha Bi. Shida, familia yake na viongozi wa Halmashauri ya Kijiji na pamoja walipitia nyaraka zote zilizotumika kugawa ardhi. Baada ya majadiliano ya muda mrefu ilibainika kuwa ardhi ambayo ilikuwa na mgogoro ilikuwa ni mali halali ya familia. Hivyo Halmashauri ya Kijiji irejeshe ardhi hiyo kwa Bi. Shida Raphael na Bw. Paulo Raphael ambao walikuwa ndio wamiliki halali.

Mnamo tarehe 16/05/2019 Halmashauri ya Kijiji cha Bonye kupitia Kamati ya Huduma za Jamii walifanya upya upimaji wa ardhi hiyo ambapo wahusika walikabidhiwa rasmi ekari 49 za ardhi waliyokuwa wanaidai. Baada ya kurudishiwa ardhi yao Bi. Shida alinukuliwa akisema yafuatayo;

> *"...Mvutano baina yangu na Halmashauri ya Kijiji ulinifanya nishindwe kuendeleza shamba kutokana na vikao vya kila mara. Niliingia gharama nyingi sana katika ufuatiliaji lakini nashukuru hatimaye nimefanikiwa kulirudisha eneo hili...".*

Wanavijiji na hususani wanawake katika Kijiji cha Bonye na vijiji jirani walipata ujasiri mkubwa kutokana na ushindi wa Bi. Shida na kaka yake Paulo na hii imeinua hamasa kwa wanavijiji kuamka na kuanza kutetea haki zao za ardhi zilizodhulumiwa miaka ya nyuma kipindi hicho wakiwa hawana uelewa wa Sheria za Ardhi.

# VICOBA YATUMIKA KUTETEA HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE

Na Tanzania Rural Women and Children Development Foundation (TARWOC)



Pichani: Wajumbe wa kikundi cha Vicoba cha Iguluba wakiwa kwenye kikao chao cha kawaida.

Vicoba ni vikundi maarufu sana vijijini na mijini, hapo awali iliaminika kuwa Vicoba ni kwajili ya wanawake tu. Ingawa kwa miaka ya karibuni kumekuwepo na mabadiliko makubwa kwasababu hata wanaume wamekuwa wakijiunga kwenye vikundi hivi. Halikadhalika imezoeleka kuwa vikundi vya Vicoba ni kwajili ya kuweka na kukopa fedha tu na sio kwajili ya kufanya masuala mengine.

Hali ni tofauti katika Kijiji cha Iguluba, Kata ya Malengamakali, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ambapo kumeanzishwa kikundi cha Vicoba ambacho pamoja na masuala ya kuweka na kukopa fedha kikundi hiki kinajihusisha na kutoa mafunzo ya masuala ya haki za ardhi kwa wanawake na wanavijiji vingine. Kikundi hiki kina jumla ya wajumbe 19 ambapo miongoni mwao kuna waliopata mafunzo kuhusu ardhi, kilimo, biashara na ujasiriamali yaliyotolewa na taasisi ya TARWOC.

Baada ya wajumbe hawa kupata mafunzo haya waliamua kuanzisha ukusanyaji wa mtaji wa fedha ili waweze kuanzisha biashara mbalimbali ikiwemo kutengeneza batiki na ufugaji wa kuku wa kienyeji. Kutokana na moyo wa hali ya juu miongoni mwa wanakikundi waliweza kukusanya fedha ambayo iliwawezesha kukodi shamba la ekari 3 ambalo wameshaliandaa kwa lengo la kulima alizeti kwajili ya kujiongezea kipato kwa mwanakikundi mmoja mmoja na kwa kikundi kwa ujumla.

Hadi kufikia mwezi Oktoba 2019 kikundi kilikuwa kimeweza kukusanya jumla ya Tsh. 3,828,000/= ambazo wameanza kukopeshana wenyewe kwa wenyewe ili kufanya maendeleo binafsi kwenye mashamba waliyonayo na familia zao. Uimara wao wa kiuchumi umeweza pia kuimarisha uhakika wa kumiliki ardhi kwa wanakikundi hawa ikiwa ni pamoja na wanawake ambao hapo kabla walishindwa kuitumia, kuilinda na kuimiliki ardhi kutokana na kukosa nguvu za kiuchumi. Mmoja wa wanakikundi Bi. Mayasa Kidope alisema yafuatayo baada ya kuhojiwa;

*"...nasikia fahari kuwa mmoja wa wanakikundi hiki kwa sababu maisha yangu yamebadilika kifikra na kiuchumi, hapo kabla nilikuwa natumia zaidi ya shilingi elfu mbili kwa siku kununua pombe za kienyeji hivyo nikaishia kuwa maskini. Kwa sasa nimeacha kabisa kupoteza fedha kwenye pombe badala yake nimejikita kwenye biashara na kilimo ili nipate fedha za kununua hisa na kurejesha mkopo ili maisha yangu na ya watoto na wajukuu yawe mazuri..."*



# WASAIDIZI WA KISHERIA WAWAJENGEA UJASIRI WANAWAKE

Na Tanzania Women Lawyers Association (TAWLA)

Katika jamii za kitanzania, wanawake wamekuwa wakidhulumiwa haki zao hasa kwenye suala la umiliki wa ardhi na mali kwa kutopewa nafasi ya kufanya maamuzi wakati uuzwaji au rehani. Kifungu cha 114 cha Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kimetoa ulinzi kwa mali ya familia kuwekwa rehani kwa kuainisha kwamba rehani ya nyumba ya familia itakuwa halali endapo itakuwa na saini inayoonesha Mke au Wake kuridhia uwekaji wa rehani wa nyumba hiyo. Vilevile kifungu cha 161(3) cha Sheria ya ardhi namba 4 ya mwaka 1999, kinaainisha kwamba kabla ya uuzwaji wa ardhi ya familia ni jukumu la mnunuzi kujiridhisha kuwa ridhaa ya mke au wake halali imepatikana. Pamoja na uwepo wa taratibu na sheria nzuri, bado jamii hususan wanawake wanaendelea kutengwa na maamuzi mengi hufanywa na wanaume pekee.




Pichani: Timu ya ufuatiliaji na tathmini ya HAKIARDHI pamoja na maafisa TAWLA na wa kituo cha TASWIRA YA HAKI

Katika kuendelea kutoa elimu, kuchochea kasi ya kutokomeza mila kandamizi na kuleta usawa katika jamii, TAWLA kupitia ufadhili wa Foundation for Civil Society kwenye mradi wa haki za ardhi na mali kwa wanawake katika jamii ya Meru, wametoa mafunzo kwa wasaidizi wa kisheria wa TASWIRA YA HAKI. Mafunzo yalihusu kuimarisha huduma ya msaada wa kisheria kwa kuzingatia taratibu na utambuzi wa wajibu wao kama inavyotambulika na *Sheria ya Msaada wa Kisheria namba 1 ya 2017.*

Wasaidizi wa kisheria hushirikiana na TAWLA kusaidia jamii hususani wanawake walio kwenye ndoa kutokana na kesi nyingi zinazohusu wanawake zinatokana na manyanyaso wanayoyapata ambazo matumizi mabaya ya mali yanayochagizwa na maamuzi ya waume peke yao katika jamii ya wameru yanachochea kasi ya manyanyaso kwa wanawake ikiwemo kupigwa na mali kuharibiwa na waume zao.

Mfano mmojawapo ni wa Bi. Rosemary Josephat mkazi wa kijiji cha Mulala Wilaya ya Meru ambaye alikuwa akinyanyasika kwa mume wake kwa kupigwa na kutoshirikishwa katika maamuzi mbalimbali ndani ya familia. Kwa kipindi kirefu cha ndoa yao, mume wake amekua akichukua mamlaka ya kuuza ardhi bila ridhaa ya mkewe. Bi. Rosemary aliweza kufika katika kituo cha msaada wa kisheria TASWIRA YA HAKI na kupata huduma ambapo TAWLA ilimsaidia kufungua kesi ya jinai dhidi ya mume wake ambapo mpaka sasa kesi inaendelea vizuri kukiwa na matumaini ya Bi. Rosemary kupata haki yake.

Kwa ujumla TAWLA imekuwa ikipokea kesi nyingi kutoka kwa wanawake wa vijijini na mijini ambao wanadhulumiwa haki zao kutokana na kutokufahamu Sheria za Ardhi kwa sababu utekelezaji wa sheria huko vijijini unafanyika taratibu sana na hivyo wanawake hawafahamu nini wafanye ili kulinda haki zao za kupata, kutumia, kumiliki, kuuza na kununua ardhi kama ambavyo wanaume walivyo na haki hizo. Manyanyaso haya kwa wanawake yanatokana na historia ya kabila la Wameru katika kusimamia mila zake na kuhakikisha kuwa mila zao zinatumika. Wasimamizi wakubwa wa mila hizi ni wanaume ambao ndani ya hizo mila kuna mila nzuri na mila kandamizi.

# WANAWAKE WA KIMAASAI WANUFAIKA NA ARDHI

Na Ujamaa Community Resource Team (UCRT)



Pichani:Bi. Magdalena akiwa na mifugo yake aliyoweza kuinunua baada ya kukodisha ardhi aliyopewa na mume wake katika Kijiji cha Lerug

Taasisi ya Ujamaa Community Resource Team inatekeleza mradi wa haki za ardhi kwa wanawake katika Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara. Jamii kubwa inayoishi kwenye wilaya hii ni Wamaasai na ni dhahiri kabisa kuwa jamii hii inaongoza kwa kuwa na mila zisizoyumba zinazosimamia wanajamii wake. Pamoja na uimara wa mila na desturi za jamii hii bado kuna mila ambazo ni kandamizi kwa wanawake, wanawake wanabanwa na mila za jamii hii katika kupata na kumliki mali ardhi ikiwa ni mojawapo ya mali hizi. Wanawake katika jamii hii hawaruhusiwi kurithi ardhi kutoka kwa wazazi wao na hata waume zao wanapofariki huwa hawana haki ya kumiliki ardhi walizozitafuta pamoja kwenye mahusiano yao.

Matumizi ya mila hizi kandamizi yameendelea kutumika kwa muda mrefu kwenye jamii hizi kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na Sheria ya Ardhi ambayo imetoa haki na wajibu kwa kila Mtanzania mwanaume na mwanamke wa kupata, kutumia na kumiliki ardhi. Hii inatokana na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zina vifungu vizuri ambavyo vinalinda na kutetea haki za wanawake. Mfano ni kifungu cha 3(2) ambacho kinaainisha ya kwamba;

*...ni haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia, kuuza au kuigawa ardhi ifahamike kuwa ni sawa sawa na haki ya mwanaume yoyote kwa viwango na masharti yaleyale...*

Vilevile, kifungu cha 20 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 kinaainisha kwamba;

*...matumizi ya mila na desturi zinazowanyima wanawake, watoto au watu wenye ulemavu njia halali za kumiliki, kukalia au kutumia ardhi ni batili...*

Pamoja na vifungu hivi vizuri bado kuna wanawake wananyanyasika kutokana na kutokufahamu haki na wajibu wao. Kwa mfano Bi. Magdalena Samweli mwenye watoto watatu, mkazi wa kijiji cha Lerug kata ya Kijungu Wilaya ya Kiteto. Yeye na mke mwenzake mdogo hapo awali hawakuwa na haki ya kupata wala kumiliki ardhi kutoka kwa mume wao.

Ilibidi hadi wanawake hawa na mume wao wapate elimu ya haki za ardhi kutoka taasisi ya UCRT ndipo walipopata nafasi ya kumshawishi na kushawishika kwa mume wake na kuamua kuwapatia wake zake ardhi wazimiliki wao wenyewe na watoto wao. Haikuwa ni rahisi kwa mume wao kukubali kuwagawia ardhi wake zake lakini kutokana na kujisomea machapisho ya haki za ardhi pamoja na kuzungumza na wakufunzi wa mafunzo haya ambao walimueleza umuhimu na faida ya kumilikisha wanawake ardhi.

Baada ya mume kukubali kugawa ardhi kwa wake zake kuliibuka mgogoro mwingine wa kiasi cha ardhi ambacho mke mkubwa anatakiwa kupata na mke mdogo anatakiwa kupata kwasababu kutokana na mila za Kimaasai mke mkubwa anatakiwa kupata zaidi ya mke mdogo. Mume wa wanawake hawa yeye alitaka kuwapatia ardhi sawa kwa sawa jambo ambalo lilileta mtafaruku mkubwa baina ya mke mkubwa ambaye alitaka kupewa ardhi kubwa zaidi kwasababu yeye ndie aliyehusika kwenye kutafuta na kuandaa mashamba hayo kwa muda mrefu kabla ya mke mdogo kuolewa.

Baada ya majadiliano ya muda mrefu mke mkubwa,Bi. Magdalena alikubali ushauri wa mume wake wa kila mmoja kupata ekari 50. Kwa kuwa Bi. Magdalena hakuwa na mtaji wa kulima eneo lote la ekari 50, aliamua alikodishe shamba lote kwa malipo ya shilingi elfu thelathini (Tsh 30,000/=) kwa ekari na kupata jumla ya shilingi milioni moja na laki tano (Tsh 1,500,000/=). Kwa kutumia pesa alizopata,Bi. Magdalena alinunua ndama jike 4, Kondoo 2, na pesa zilizobaki aliagiza nguo za kimaasai za kuuza nyumbani pamoja na kufungua duka la bidhaa za rejareja ambalo anamiliki yeye pamoja na mdogo wake. Biashara na amani aliyo nayo kwa kumilikishwa ardhi kisheria imebadilisha maisha yake kijamii na kiuchumi. Bi. Magdalena alipohojiwa alisema yafuatayo;

*“...maisha yangu yamebadilika sasa naweza kujitegemea na kuhimili ugumu wa maisha, nafurahi sana sababu sisi wanawake wa Kimaasai tunachukuliwa kama watoto lakini sasa nimekuwa mfano bora wa maendeleo kwa wanawake wenzangu...*



# MILA KANDAMIZI KIKWAZO KWA WANAWAKE KUMILIKI ARDHI

*Na Women Development for Science and Technology (WODSTA)*

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinatambua usawa na haki za kila Mtanzania katika kupata, kutumia na kumiliki mali ikiwa ni pamoja na ardhi na rasilimali zake. Pamoja na Katiba na Sheria hizi kutokuwa na ubaguzi lakini bado kuna mila na desturi za makabila mengi hapa nchini ambazo hazimpi mwanamke fursa ya kumiliki mali na ardhi. Katika makabila haya mila na desturi hazimruhusu mwanamke humiliki ardhi moja kwa moja bali kupitia kwa mume wake, watoto wake wa kiume, ndugu zake wa kiume au shimeji zake pindi mumewe anapofariki.

Ingawa katika ngazi ya familia na ukoo, mwanamke ana haki ya kutumia ardhi kwa shughuli za uzalishaji kama vile kilimo na ufugaji na wanawake ndio wazalishaji wakubwa kwenye familia. Ila kwa kutokuwa na haki ya umiliki wa ardhi, mwanamke amekuwa akikosa maamuzi katika mazao yatokanayo na ardhi aliyolima. Mila na desturi zimempa mwanaume sauti na maamuzi hata katika kile kinachozalishwa shambani.

Kufuatia changamoto hii taasisi ya WODSTA inatekeleza mradi wa haki za ardhi katika kijiji cha Lemanda kilichopo kata ya Oldonyosambu katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Miongoni mwa wanufaika wa mradi huu ni viongozi wa mila na wanawake wajane ambao kwa pamoja walipatiwa mafunzo juu ya umuhimu na haki ya kumiliki ardhi kwa wanawake.

Mzee Loishiye Joseph, ambaye ni Laigwanani wa Jamii ya Wamaasai mwenye umri wa miaka 75 katika alipata mafunzo ya haki za ardhi kwa wanawake. Mara tu baada ya mafunzo amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba analinda na kutetea haki za umiliki ardhi kwa wanawake ikiwa ni pamoja na kusambaza elimu aliyoipata kwa viongozi wengine wa kimila kupitia mikutano yao. Kwa mfano Mzee Loishiye amefanikiwa kuwasaidia wajane wawili kurejeshewa ardhi yenye ukubwa wa ekari 2 kwa kila mmoja. Wajane hawa ni Bi. Naseriani Edward (39) na Bi. Adelina Simon (47) ambao walinyang'anywa ardhi na shemeji zao baada ya kufiwa na waume zao.



*Pichani: aliyesimama ni Laigwanani wa Wamaasai, Mzee Joseph Loishiye Kijiji cha Lemanda*



Kabla ya wajane hawa kupata haki yao walipitia matatizo na manyanyaso makubwa hali iliyowasababishia msongo wa mawazo na kuwadhoofisha kiuchumi kutokana na kukosa ardhi ya kilimo. Kutokana na kulelewa katika mila kandamizi hawakupata ujasiri wa kuwafungulia kesi shimeji zao kwasababu wangetengwa na familia zao kwa kufanya tukio la aibu. Hivyo waliamua kupambana kimya kimya pasipo kuwa na msaada wowote kwa kipindi chote. Mafunzo ya haki za ardhi kwa viongozi wa kimila na vijiji ndio yaliyokuwa msaada kwa wajane hawa baada ya kupata nafasi ya kueleza matatizo yao na kusikilizwa na wazee wa kimila ndipo tatizo lao lilipopata ufumbuzi. Mzee Loishiye Joseph alifanikiwa kuwakutanisha viongozi wengine wa mila, ndugu za wajane walioshtakiwa pamoja na wajane wenyewe. Baada ya majadiliano, kikao kiliamuru wajane hao warudishiwe ardhi yenye ukubwa wa ekari mbili kwa kila mmoja. Makubaliano na agizo hilo yaliwekwa katika maandishi na kusainiwa na pande zote.

Kwa sasa,Bi. Adelina na Bi. Naseriani wamefanikiwa kulima na kufuga katika mashamba waliyorudishiwa ambako wanalima mazao ya chakula na biashara na kuendeleza familia zao. Mzee Loishiye baada ya kuhakikisha kuwa wanawake hawa wamepata haki yao alisema yafuatayo;

> *"…Wazee wa mila hatupo tena nyuma tumeshtuka, pamoja na kulinda haki za akina mama mimi binafsi nimeandika urithi sawa kwa watoto wangu wote wa kike na kiume…"*



*Pichani: Adelina Simon (47) kwenye shamba alilorejeshewa*



*Pichani: Naseriani Edward (39) akiwa kwenye sehemu ya shamba alilorejeshewa*

# NAFASI YA WANAWAKE KATIKA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

*Na HAKIARDHI*




Sheria ya Ardhi namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 za mwaka 1999 zimetungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Sheria hizi zinaainisha vyombo vyenye dhamana ya utatuzi wa migogoro ya ardhi na nyumba katika mfumo wa kiutawala na kimahakama. Lengo la kuwapo kwa mifumo hii ni kumwezesha na kumrahishia mzalishaji mdogo hususani wanawake, walemavu na wengine wasiokuwa na uwezo wa kukimbizana na kesi katika vyombo vya juu vya kimahakama kutokana na sababu za gharama za safari na malazi pamoja na kuwalipa wanasheria.

Katika ngazi ya kijiji chombo cha kiutawala kilichopo ni Kamati ya Uamuzi wa Kijiji na chombo cha kiusuluhishi ni Baraza la Ardhi la Kijiji. Vilevile kuna vyombo vingine vya kimahakama katika ngazi ya Kata na Wilaya ambavyo ni Baraza la Kata na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Halikadhalika katika ngazi ya kitaifa kuna Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania.

Mfumo huu wa utatuzi wa migogoro ya ardhi wa Mabaraza na Mahakama katika ngazi ya Kijiji, Kata na Wilaya umefafanuliwa kwa kina katika sheria ya Mabaraza na Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya mwaka 2002 iliyoanza kutumika tarehe 1/10/2003. Sheria hii ilifuta mamlaka ya Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi kusikiliza na kuamua masuala yote ya madai kuhusu ardhi. Vilevile inafuta Mabaraza ya Nyumba ya Mikoa, Baraza la Rufaa la Nyumba, Mabaraza ya Usuluhishi wa Ardhi ya Wilaya na Mikoa na Baraza la Rufaa la Ardhi. Sheria hii iliunda na inatoa majukumu na mamlaka ya Mahakama zilizotajwa katika Sheria Namba 4 na 5 za mwaka 1999 kushughulikia migogoro ya ardhi na nyumba.

Nafasi ya wanawake katika mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi imeainishwa katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na uteuzi na uchaguzi wa wajumbe, akidi ya wajumbe wanaoweza kufanya maamuzi pamoja na ushiriki wa wanawake katika kila hatua ya usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwa mfano, Kamati ya Uamuzi wa Kijiji wajumbe wake wanapendekezwa na Halmashauri ya Kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji chini ya kifungu cha 53 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya 1999. Kamati hii inahusika na usuluhishi wa migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi, haki za njia na maslahi ya wanawake, walemavu, na watu wasiokuwepo kijijini. Kamati hii ina wajumbe 9, wajumbe wanawake wasipungue 4. Wajumbe wa kamati hii watadumu kwa kipindi cha miaka 3 na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka 3. Kikao halali cha Kamati hii kinatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua 5, ambapo 2 kati yao ni lazima wawe wanawake.

Kwa upande wa mfumo wa mahakama, ngazi ya awali ni Baraza la Ardhi la Kijiji lenye jukumu la kusuluhisha migogoro yote ya ardhi kijijini. Baraza hili linaundwa na wajumbe 7 kati yao wanawake wasipungue 3. Wajumbe wa Baraza hili wanateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Kikao halali cha Baraza hili kinatakiwa kiwe na wajumbe 4 ambapo 2 lazima wawe wanawake.

Ngazi inayofuata ni ngazi ya Kata ambapo kuna Baraza la Kata linaloundwa na wajumbe 8 kati yao wanawake wasipungue 3. Wajumbe hawa wanateuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985. Mwenyekiti wa Baraza huchaguliwa miongoni mwa wajumbe. Katibu wa Baraza ni mwajiriwa wa Halmashauri ya Wilaya na sio mjumbe wa Baraza bali ni Katibu wa Baraza tu.

Katika ngazi ya Wilaya kuna Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya linaloongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Mwanasheria kwa taaluma. Mwenyekiti huajiriwa na Wizara ya Ardhi kwa kuzingatia vigezo vya ajira. Mwenyekiti wa Baraza hili husaidiwa na Wazee wa Baraza 7 ambapo 3 kati yao ni wanawake wanaoteuliwa na Waziri wa Ardhi kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa ambapo wilaya inapatikana.

Katika ngazi ya juu kuna Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani inayoongozwa na majaji. Miongoni mwa majaji waliopo kuna kuna Majaji wanawake katika vyombo hivi hivyo sheria haijabagua jinsi katika mfumo wa kutatua migogoro ya ardhi nchini. Sheria zote zinasisitiza nafasi ya mwanamke katika vyombo hivi kwa lengo la kuhakikisha kuwa maslahi ya wanawake katika ardhi yanalindwa ipasavyo.



LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

TOLEO LA 3 | MACHI 2020




Mradi huu unafadhiliwa na Foundation for Civil Society

FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
*Facilitating Partnerships for Development*